

Obadia

Contents

Obadia

1Maono ya Obadia.

H ili ndilo asemalo Bwana Mwenyezi kuhusu Edomu:

T umesikia ujumbe kutoka kwa Bwana:

M jumbe alitumwa kwa mataifa kusema,

“ Inukeni, twendeni tukapigane vita dhidi yake.”

2“Angalieni, nitawafanya wadogo miongoni mwa mataifa,

m tadharauliwa kabisa.

3Kiburi cha moyo wako kimekudanganya,

w ewe unayeishi katika majabali ya miamba

n a kufanya makao yako juu,

w ewe unayejiambia mwenyewe,

‘ Ni nani awezaye kunishusha chini?’

4Ingawa unapaa juu kama tai

n a kufanya kiota chako kati ya nyota,

n itakushusha chini kutoka huko,” asema Bwana.

5“Ikiwa wevi wangukuja kwako,

i kiwa wanyang’anyi wangukujia usiku:

L o! Tazama ni maafa kiasi gani yangukuwa yanakungojea:

j e, si wangeiba tu kiasi ambacho wangehitaji?

- K** ama wachuma zabibu wangekuja kwako,
j e, wasingebakiza zabibu chache?
- 6Lakini tazama jinsi Esau atakavyotekwa,
j insi hazina zake zilizofichwa zitatekwa nyara!
- 7Wote uliungana nao watakufukuza hadi mpakani,
r afiki zako watakudanganya na kukushinda,
w ale wanaokula mkate wako watakutegea mtego,
l akini hutaweza kuugundua.
- 8“Katika siku hiyo,” asema Bwana,
“ je, sitaangamiza watu wenye hekima wa Edomu,
w atu wenye ufahamu katika milima ya Esau?
- 9Ee Temani, mashujaa wako watatiwa hofu,
k ila mmoja katika milima ya Esau
a taangushwa chini kwa kuchinjwa.
- 10Kwa sababu ya jeuri uliyofanya dhidi ya ndugu yako Yakobo,
a ibu itakufunika;
u taangamizwa milele.
- 11Siku ile ulisimama mbali ukiangalia
w akati wageni walipojichukulia utajiri wake
n a watu wa nchi nyingine walipoingia malango yake

w akipiga kura kwa ajili ya Yerusalemu,

u likuwa kama mmoja wao.

12Usingemdharau ndugu yako

k atika siku ya msiba wake,

w ala kufurahia juu ya watu wa Yuda

k atika siku ya maangamizi yao,

w ala kujigamba sana

k atika siku ya taabu yao.

13Usingeingia katika malango ya watu wangu

k atika siku ya maafa yao,

w ala kuwadharau katika janga lao

k atika siku ya maafa yao,

w ala kunyang'anya mali zao

k atika siku ya maafa yao.

14Usingengoja kwenye njia panda

n a kuwaua wakimbizi wao,

w ala kuwatoa watu wake waliosalia

k atika siku ya shida yao.

15“Siku ya Bwana iko karibu

k wa mataifa yote.

K ama ulivyofanya, nawe utafanyiwa vivyo hivyo,

m atendo yako yatakurudia juu ya kichwa chako.

16Kama vile ulivyokunywa juu ya mlima wangu mtakatifu,

v ivyo hivyo mataifa yote watakunywa mfululizo,

w atakunywa na kunywa,

n ao watatoweka kana kwamba hawajawahi kuwepo.

17Lakini katika Mlima Sayuni kutakuwepo

n a wale watakaookoka;

n ao utakuwa mtakatifu,

n ayo nyumba ya Yakobo

i tamiliki urithi wake.

18Nyumba ya Yakobo itakuwa moto,

n a nyumba ya Yosefu itakuwa mwali wa moto;

n ayo nyumba ya Esau itakuwa bua kavu,

n ao wataiwasha moto na kuiteketeza.

H akutakuwa na watakaosalimika

k utoka nyumba ya Esau.” Bwana amesema.

19Watu kutoka nchi ya Negebu

w ataikalia milima ya Esau,

n a watu kutoka miteremko ya vilima

w atamiliki nchi ya Wafilisti.

W atayakalia mashamba ya Efraimu na Samaria,

n aye Benyamini atamiliki Gileadi.

20Kundi la Waisraeli walioko uhamishoni Kanaani

w atarudi na kumiliki nchi mpaka Sarepta.

W alioko uhamishoni Sefaradi kutoka Yerusalemu

w atamiliki miji ya Negebu.

21Waokoaji watakwea juu ya Mlima Sayuni

k utawala milima ya Esau.

N ao ufalme utakuwa wa Bwana.